

Maswali

1. Farao aliambia Yusufu afanye nini?
2. Yusufu aliwapa nini ya safari?
3. Yusufu alifanya nini alipokutana na Yakobo?
4. Yakobo najamii yake waliishi wapi?
5. Yakobo alikuwa na umri gani alipoenda Misri?
6. Watu wa Misri walimpea Yusufu nini ili wapate chakula?
7. Walipeana nini walipoishiwa na pesa?
8. Yusufu aliwapa watu nini ili wakuze chakula?
9. Jamii ya Yakobo walioenda Misri walikuwa wangapi?
10. Yakobo alipopelekwa kwa Farao, alimfanyia nini?

Majibu

1. Farao alimwambia Yusufu amlete Yakobo.
2. Yusufu aliwapa magari na chakula wale njiani.
3. Yusufu alilia kwa furaha alipokutana na Yakobo.
4. Yakobo najamii yake waliishi Gosheni huko Misri.
5. Yakobo alikuwa na umri wa miaka mia moja thelathini wakati alienda Misri.
6. Watu wa Misri walipea Yusufu pesa ili wapate chakula.
7. Walipoishiwa na pesa walipeana mifugo na nchi pia.
8. Yusufu aliwapa mbegu ili wakuze chakula.
9. Jamii ya Yakobo walioenda Misri walikuwa 70.
10. Yakobo alipopelekwa kwa Farao alimbariki

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

13 Yakobo anaenda Misri

Marejeo

Mwanzo 46 & 47

Kiini cha somo

Kuonyehsa upendo na ulinzi Mungu kwa kila mtu

Maneno maalum

- 1 Ndugu wa Yusufu wanaenda Misri + Farao anaambia Yusufu alete jamii yake + Yusufu anapeleka chakula na magari
- 2 Yusufu yu hai + Yakobo anafuraha + Yakobo aenda Misri
- 3 Yusufu afurahi kukutana na Yakobo + Nduguze wakutana na Farao + jamii ya Yusufu wanaishi Gosheni
- 4 Njaa + watu wananunua chakula + uza mifugo kwacehakula tena + Yusufu ananunua mashamba + Yusufu anabadilisha mbegu kwa chakula
- 5 Jamii ya Yakobo yaongezeka

13.1 Ndugu wa Yusufu walikuja Misri kununua chakula wakati wa njaa. Yusufu alifurahi kuwaona. Farao alimwambia Yusufu alete babake Yakobo kutoka nchi ya Kanaani." Leta babako Misri na jamii yote," Farao alisema, "na nitawapa nchi nzuri'.

Yusufu alipea nduguze magari na chakula wale njiani. Ndugu wake Yusufu walirudi Kanaani kuleta baba yao.

13.2 "Yusufu angali hai," walimwambia Yakobo, "na yeye ndie mtawala wa Misri." Yakobo alifurahi alipojua Yusufu yu hai. "Yusufu mwanangu angali hai!" akasema kwa mshangao. "Nitaenda nimwone kabla sijafa."

Yakobo na jamii yake walisafiri kwenda Misri. Walichukuwa mifugo na mali yao yote. Jamii ya Yakobo walikuwa watu sabini walipoenda Misri

13.3 Yusufu aliposikia wanakuja, alipanda gari na kwenda kumlaki babake Yakobo. Yusufu alimuangukia Yakobo shingoni na kulia kwa furaha alipomuona. Alichukua nduguze watano kuenda kuona Farao.



Farao alisema, "Muende muishi Gosheni na nitawafanya wachungaji wakuu juu ya mifugo yangu yote pia." Baadaye Yusufu alipeleka babake kwa Farao na Farao akabarikiwa na Yakobo.

"Una umri gani?" Farao alimuuliza Yakobo. "Nina miaka mia moja thelathini," Yakobo alisema. Baba wa

Yusufu na ndugu zake waliishi katika nchi ya Gosheni iliyokuwa nzuri sana hapo Misri.

13.4 Hakukuwa na chakula kwa nchi yote sababu kulikuwa na njaa nyingi vile Mungu alikuwa amesema. Lakini Yusufu aliwapa jamii yake chakula, tena aliwauzia wamisri. Walipokosa pesa, walimwendea na kusema, "Tupe chakula na bure tutakufa, hatujabaki na pesa."

Yusufu alisema, "Mpe Farao mifugo na nitampea chakula." Kwa hivyo, watu walileta mifugo na wakapewa chakula.

Mwaka uliofuata, watu walikuja tena na kusema, "Pesa yetu imekwisha, na mifugo yetu imekwisha, hakuna kilichobaki isipokuwa nchi yetu."

Yusufu alimnunulia Farao nehi yote ya Misri. Akawapa chakula kwa sababu njaa ilikuwa nyingi sana. Kwa hivyo, nchi yote ya Misri ikawa ya Farao. Njaa ilipoisha, Yusufu aliwapa mbegu ya kupanda na wakawa na chakula tena.

13.5 Yakobo alikuja kwa nchi ya Misri na jamii yake. Jamii ilikua mpaka wakawa wengi zaidi na kujaza nchi.

